# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.21. Msimu wa Kilimo 2022/23* *Tathmini ya Aprili 21-30, 2023 na Matazamio kwa Kipindi cha Mei 1-10, 2023*



**MUHTASARI**

- Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi yanayopata mvua za Msimu inatarajiwa kusaidia kukomaa kwa mazao hususan mahindi
- Unyevu mwingi wa udongo unaweza kuzorotesha shughuli za kilimo, ukuaji na maendeleo ya mazao kutokana na mashamba kujaa maji hususan katika maeneo ya pwani ya kaskazini na ukanda wa ziwa Viktoria
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani na kutumia taarifa za hali ya hewa katika shughuli zao za kila siku.


## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2023


Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia iliimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia haikuwa na mabadiliko. Hali hii iliendelea kuuweka ukanda mvua (ITCZ) katika maeneo ya kaskazini mwa nchi.

Joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikua la juu kidogo ya wastani na hivyo kuwa na mchango kwa unyevunyevu kuelekea ukanda wa pwani. Katika eneo la tropiki ya kati ya bahari ya Pacific joto la bahari lilikua la juu kidogo ya wastani. Hali hii ilikuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha mifumo ya kutengeneza mvua nchini.

Kwa upande mwingine, joto la bahari mashariki mwa bahari ya Atlantic (pwani ya Angola) lilikua la juu ya wastani na hivyo kuwa na mchango hafifu kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2023

Katika kipindi hiki maeneo mengi nchini yamepata mvua kati ya 50 mm na 150 mm. Kiasi kikubwa zaidi cha mvua (milimita 435) ilinyesha katika maeneo kituo cha hali ya hewa kilimo Lyamungu mkoani Kilimanjaro kama inavyooneshwa katika Kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Aprili 21-30, 2023

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2023

Mvua zilizonyesha katika dekadi hii, zimesaidia ukuaji na maendeleo ya mazao katika maeneo yanayopata mvua masika na Msimu.

Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka hususan mikoa ya Njombe, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Tabora na Kigoma (kusini), mahindi yalikuwa katika hatua ya kukomaa.

Aidha, zao la mahindi katika maeneo yanayopata mvua za masika yapo katika hatua ya kati ya jani la tatu na la tisa, na wakulima wameendelea na palizi na matumizi ya viuatilifu.

Zao la mpunga lipo katika hatua ya kuchanua katika maeneo ya mikoa ya Morogoro kusini, Tabora, Mbeya na

Rukwa.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo ulikuwa wa kuridhisha katika maeneo mengi nchini kutokana na mvua zinazoendelea.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2023

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito na mabonde kiliongezeka kutokana na mvua zilizonyesha isipokuwa maeneo ya mikoa ya kati ambako mvua za msimu zinaelekea mwisho..

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2023

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kuuruhusu ukanda mvua (ITCZ) kuelekea kaskazini zaidi mwa nchi.

Joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani, hali inayotarajiwa kuwa na mchango mdogo katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea maeneo ya pwani.

Katika eneo la tropiki ya kati ya bahari ya Pacific joto la bahari linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani. Kwa upande mwingine, joto la bahari mashariki mwa bahari ya Atlantic (pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la juu ya wastani na hivyo kuwa na mchango hafifu katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2023

Maeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kupata mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) inatarajiwa kuwa na mvua.

Maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi), na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2023

Hali ya unyevunyevu kwenye udongo inatarajiwa kuendelea kuongezeka hususan katika maeneo ya pwani ya kaskazini na kanda ya ziwa Viktoria kutokana na mvua zinazotarajiwa.

Hata hivyo, unyevunyevu uliokithiri na kujaa maji katika mashamba unaweza kuzorotesha shughuli za kilimo, ukuaji na maendeleo ya mimea.

Kwa upande mwingine, hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi yanayopata mvua za Msimu inatarajiwa kusaidia kukomaa kwa mazao hususan mahindi.

Wakulima na maafisa ugani wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao na mashamba ili kuweza kukabiliana na athari zinazoweza kutokana na unyevunyevu wa udongo wa kupitiliza na milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea pale vitakapojitokeza.

Jamii za wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye baharini ya Hindi na maziwa makuu ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi. Wafugaji pia wanashauriwa kuhakikisha mifugo yao inalindwa dhidi ya hali mbaya ya hewa na magonjwa ya mlipuko.

Kwa ujumla, inashauriwa kuzingatia utabiri wa hali ya hewa katika shughuli na mipango ya kila siku.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2023

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa vya kawaida. Hata hivyo, jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kadiri inavyowezekana kwa ajili ya matumizi ya baadae.



Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)